**Issue no:** 01 | **Vol no:** 07 | **January** 2026: 13-25

# Udhihirikaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu katika Tamthilia ya *Shamba la Halaiki*

**Ogonda Samuel Sinzore**

Kibabii University, Kenya.
Author's email: sasio.ogonda@gmail.com

**Article History**
Received: **2025.11.18**
Accepted: **2025.12.22**
Published: **2026.01.13**

**Cite this article in APA**
Ogonda, S.S. (2026). Udhihirikaji wa malengo ya maendeleo endelevu katika tamthilia ya *Shamba la Halaiki*. *Editon consortium journal of kiswahili*, *7*(1), 13-25. https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v7i1.695

**Ikisiri**

Lengo la makala hii ni kuchunguza udhihirikaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu (MME) katika tamthilia ya *Shamba la Halaiki* (Okello, 2016). Mpango wa MME umekumbatiwa na wasomi, wataalamu, mashirika na serikali mbalimbali duniani kwa kuwa ni njia ya kuafikia maendeleo. Waandishi wa fasihi wameshughulikia masuala ya maendeleo katika kazi zao. Fasihi kupitia utanzu wa tamthilia ina nafasi muhimu ya kuchangia uafikiaji wa MME kwa kuyaangazia. Utafiti huu ni wa kithamani na uliongozwa na Nadharia ya Uhistoria Mpya iliyoasisiwa na Stephen Greenblatt (1980) na kuendelezwa na Brizee na Tompkins (2012). Muundo wa kiuchanganuzi ulitumiwa. Data ilikusanywa kupitia mbinu ya unukuzi. Data kuhusu namna MME yanavyodhihirika katika tamthilia teule iliibuliwa kupitia wahusika, uumbaji wa mandhari na maudhui. Data hii ilipangwa kisha kuchanganuliwa kwa njia ya uhakiki wa yaliyomo. Kwa kutumia mbinu ya usampulishaji dhamirifu, tamthilia ya *Shamba la Halaiki* iliyoandikwa na Daniel Okello, 2016 iliteuliwa. Tamthilia hii iliteuliwa kwa msingi kuwa inaangazia MME na imeandikwa kati ya miaka ya 2016 na 2026 ambao ni kipindi cha utekelezaji wa mpango wa MME. Matokeo yamewasilishwa kwa njia ya maelezo ya maandishi. Matokeo yanaonyesha kuwa tamthilia teule inadhihirisha MME kupitia vipengele vya kifasihi kama wahusika, mandhari na maudhui, hivyo kujitokeza kama jukwaa muhimu la kujadili maendeleo ya kijamii, kiuchumi na kimazingira. Hata hivyo, imebainika kuwa baadhi ya malengo hayajaangaziwa ipasavyo, hususan L2, L8, L9, L10, L12 na L14. Makala inapendekeza waandishi wa fasihi kuzingatia zaidi malengo haya ili kuimarisha mchango wa fasihi katika kuendeleza ajenda ya maendeleo endelevu.

**Key words**: Maendeleo, mabadiliko ya tabianchi, Malengo ya Maendeleo Endelevu (MME), tamthilia, uongozi.

Editon OPEN ACCESS

This article is distributed under the license of a Creative Commons Attribution-Non Commercial-ShareAlike 4.0 International License. It is permitted to be used, reproduced and distributed in line with Editon Consortium Publishing guidelines.

## UTANGULIZI

Fasihi ni muhimu katika utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu (MME) (Havaldsen, 2020; Alcántara et al., 2020). Licha ya umuhimu wa MME katika maendeleo ya jamii, bado haijabainika kwa kina namna tanzu za fasihi ya Kiswahili, hususan tamthilia, zinavyochangia malengo haya. Makala hii iliangazia udhihirikaji wa MME katika tamthilia teule za Kiswahili. MME ni mpango ulioidhinishwa na nchi wanachama wa UM Septemba mwaka 2015 (Barbier & Burgess, 2017). Mpango huu unalenga kuafikia maendeleo ya kijinsia, usawa wa kimazingira na ukuaji wa kiuchumi. MME ni ajenda ya kimataifa iliyo na malengo 17, shabaha 169 na viashiria 232 (Gosling-Goldsmith, 2018). Kwa mujibu wa Griggs et al. (2017), malengo haya yamefumwa pamoja. Malengo na michomo hii inahusiana na kukamilishana (Magendane & Kapazoglou, 2021).

Mazza (2021) anashadidia kwamba, MME yamekuwa eneo la kuangazia si tu katika uwanja wa kiakademia bali pia katika mipango ya maendeleo ya mataifa mbalimbali. Mensah (2019) anasema kuwa MME yamevutia umakini mkubwa kutoka kwa wasomi, watawala na waratibu wa mipango. Mashirika mbalimbali ya kiserikali na yasiyo ya kiserikali yameonekana kukumbatia MME kama dhana faafu ya kimaendeleo.

Katika utekelezaji, shirika la UM kupitia kwa lengo la 17 la mpango wa MME linasisitiza umuhimu wa ushirikiano katika kuafikia MME (Browne & Millington, 2015). Ushirikiano mojawapo ni baina ya taaluma mbalimbali. Tafiti mbalimbali zimebainisha namna fasihi inavyoweza kuhusishwa kuleta maendeleo na kuendeleza uafikiaji wa MME (Havaldsen, 2020; Edler & Park, 2021).

Tamthilia ni mojawapo ya tanzu za fasihi. Kulingana na Mlama (1991), tamthilia hujitokeza kupitia mazungumzo ya moja kwa moja na matendo ya wahusika. Tamthilia ina uwezo wa kuonyesha uhalisia wa jamii kwa njia ya moja kwa moja na ya kugusa hisia za hadhira au wasomaji. Hii inatokana na hali kwamba, hoja katika tamthilia huwasilishwa kupitia migogoro, mivutano, na maingiliano ya moja kwa moja baina ya wahusika (Mazrui na Mazrui, 1995). Tamthilia ina uwezo wa kipekee wa kuwasilisha masuala ya kijamii kama vile uongozi, maadili, dhuluma, ukandamizaji, na maendeleo ya jamii kwa njia ya wazi na yenye mvuto (Mazrui & Mazrui, 1995; Mlama, 1991). Kazi hii ilishughulikia namna Daniel Okello alivyoangazia suala la MME katika kazi yake. Ni kuangazia huku ndiko kunakochangia uafikiaji wa MME. Kazi hii ina umuhimu kwa kuwa inapanua uelewa wa nafasi ya fasihi katika masuala ya maendeleo na kutoa msingi wa tafiti zaidi kuhusu uhusiano kati ya fasihi na MME katika muktadha wa Kiafrika. Makala hii ilihusisha sehemu ya utangulizi, mapitio ya maandishi, mbinu za utafiti, matokeo na hatimaye hitimisho na mapendekezo.

## MAPITIO YA MAANDISHI

Sehemu hii inahakiki tafiti mbalimbali zinazohusiana na Malengo ya Maendeleo Endelevu (MME) na fasihi, kwa lengo la kuonesha mchango wake katika utafiti huu pamoja na kubainisha pengo la utafiti lililopo.

Musindalo (2020) alipochunguza taswira ya haki za watoto katika riwaya za Kiswahili, alionyesha uhusiano wa moja kwa moja kati ya masuala ya haki za kijamii na MME, hususan Lengo la 4 na 11. Ingawa utafiti wake unatoa msingi muhimu wa kuelewa jinsi fasihi inavyoweza kuakisi masuala ya maendeleo, umejikita zaidi katika riwaya na haki za watoto, bila kugusia kwa kina namna tamthilia za Kiswahili zinavyowasilisha MME kwa upana wake. Hivyo basi, utafiti huu unapanua mjadala huo kwa kuangazia tamthilia ya *Shamba la Halaiki* (Okello, 2016).

Taylor (2016) anaeleza kuwa MME ni mwendelezo wa Malengo ya Milenia Mpya (MMM) na unalenga kuziba mapengo yaliyobaki katika utekelezaji wake. Hoja hii ina umuhimu katika utafiti huu kwa kuwa inaonesha msingi wa mageuzi ya ajenda ya maendeleo, ambayo katika muktadha wa fasihi huweza kuakisiwa kupitia migogoro na dhamira katika tamthilia za Kiswahili. Hata hivyo, tafiti hizi hazijachunguza kwa kina jinsi mageuzi haya yanavyojitokeza kisanaa katika kazi maalum za kifasihi kama tamthilia.

Aidha, Havaldsen (2020) amebainisha kuwa fasihi ina uwezo wa kubadilisha mitazamo ya jamii kuhusu maendeleo kwa kuchochea tafakuri ya kina. Dhana hii ina umuhimu katika utafiti huu kwa kuwa inasaidia kuelewa jinsi tamthilia za Kiswahili, kama *Shamba la Halaiki*, zinavyotumia wahusika na migogoro kuibua changamoto za kijamii zinazohusiana na MME. Hata hivyo, tafiti nyingi za aina hii zimebaki katika kiwango cha nadharia ya jumla bila kuchunguza matini maalum za fasihi ya Kiswahili.

Vilevile, Edler & Park (2021) wanaeleza kuwa utamaduni na fasihi ni nyenzo muhimu katika

kuhamasisha mabadiliko ya kijamii na kufanikisha MME. Hoja hii inaimarisha msingi wa utafiti huu kwa kuwa tamthilia za Kiswahili huakisi maadili, changamoto na matumaini ya jamii. Hata hivyo, bado kuna pengo la kitaaluma katika kuonyesha kwa mifano ya moja kwa moja jinsi tamthilia mahususi zinavyotekeleza jukumu hili.

Isitoshe, Alcántara et al. (2020) walidhihirisha kwamba fasihi inaweza kutumika kama nyenzo ya kufundishia na kuelewa MME kupitia uchambuzi wa wahusika na matukio. Ingawa utafiti wao unathibitisha uwezo wa fasihi katika elimu ya maendeleo, umejikita katika riwaya ya Kiingereza (*Harry Potter*) na si katika fasihi ya Kiswahili. Hivyo basi, kuna haja ya kuchunguza namna tamthilia za Kiswahili zinavyoweza kutimiza jukumu hilo katika muktadha wa Kiafrika.

Kwa ujumla, tafiti hizi zinakubaliana kuwa fasihi ni chombo muhimu katika kuwasilisha na kuendeleza MME. Hata hivyo, zinaonesha upungufu wa tafiti zinazochunguza kwa kina tamthilia za Kiswahili kama jukwaa la MME. Pengo hili ndilo linalozibwa na makala haya, ambayo yanachunguza namna MME yanavyodhihirika katika tamthilia ya *Shamba la Halaiki* (Okello, 2016).

**Nadharia ya Utafiti**

Kazi hii iliongozwa na nadharia ya Uhistoria Mpya iliyoasisiwa na Stephen Greenblatt (1980) na kuendelezwa na Brizee & Tompkins (2012). Nadharia hii ina mihimili mitatu mikuu. Mhimili wa kwanza ni kuwa masuala ya kifasihi huzingatia wakati au muhula na mahali. Wa pili ni utunzi wa kazi ya fasihi na jamii ambayo kwayo kazi hiyo imeandikwa ni muhimu, na wa tatu ni kuwa fasihi inaweza kuelezwa nje ya mtungo wenyewe. Mhimili wa pili: utunzi wa kazi ya fasihi na jamii ambayo kwayo kazi hiyo imeandikwa ni muhimu ulifaulisha kazi hii. Kupitia kwa mhimili huu, vipengele vya utunzi wa fasihi vikiwemo fani na maudhui vimetumiwa kubainisha MME katika tamthilia teule.

## MBINU ZA UTAFITI

Utafiti huu ni wa kithamani na ulitumia muundo wa kiuchanganuzi. Kwa mujibu wa Mwanje (2001), mkabala huu ni faafu kwa makala ya kimatini. Muundo huu ulitumiwa kuchanganua suala la MME katika tamthilia teule. Mbinu ya usampulishaji kidhamirifu ilitumiwa kuteua tamthilia ya *Shamba la Halaiki* (Okello, 2016). Data ilikusanywa maktabani kupitia usomaji wa kina wa tamthilia teule. Mbinu ya ukusanyaji data iliyotumika ni usomaji wa maandishi ya kifasihi. Tamthilia zilichunguzwa kwa makini ili kubaini vipengele vinavyohusiana na MME. Katika mchakato huo, data ilitambuliwa na kubainishwa kwa kutumia orodha ya uthibitishaji iliyojumuisha: wahusika, mandhari na maudhui yanayohusiana na MME. Orodha hii ilitumika kama mwongozo wa kuhakikisha kuwa vipengele vyote muhimu vinavyohusiana na malengo ya utafiti vinatambuliwa kwa usahihi na kwa uthabiti katika tamthilia zilizoteuliwa. Baada ya ukusanyaji, data ilipangwa kwa utaratibu na kisha kuchanganuliwa kwa kutumia mbinu ya uhakiki wa yaliyomo. Hatimaye, matokeo ya utafiti yamewasilishwa kwa njia ya maelezo ya kitaaluma.

Masuala ya kimaadili yamepewa kipaumbele katika kazi hii. Creswell (2003) anaibua hoja kuwa, katika uandishi na usambazaji, mtafiti hafai kudanganya, kuzima au kubatilisha matokeo ya utafiti ili kutimiza mahitaji yake au ya hadhira. Usahihi wa matokeo umezingatiwa kwa kuhakikisha kuwa matokeo hayabatilishwi kwa vyovyote vile. Kila kazi iliyosomwa na kurejelewa katika makala haya imetambuliwa. Haki miliki za watunzi zimezingatiwa kwa kuhakikisha kuwa yaliyoandikwa katika vitabu vilivyotumiwa katika utafiti huu hayapunguzwi au kuongezwa. Unukuzi kutoka kwa tamthilia teule umefanywa kwa kurejelea kurasa maalumu na pia bila kuongeza maneno yoyote ambayo hayapatikani katika tamthilia hizi.

## MATOKEO YA UTAFITI

### Malengo ya Maendeleo Endelevu katika Tamthilia Teule za Kiswahili

Tamthilia ina uwezo wa kipekee wa kuwasilisha masuala ya kijamii kama vile uongozi, maadili, dhuluma, ukandamizaji, na maendeleo ya jamii kwa njia ya wazi na yenye mvuto (Mazrui & Mazrui, 1995; Mlama, 1991). MME ni ajenda ya kimataifa iliyo na malengo 17 ambayo yamefumwa pamoja (Griggs et al., 2017; Gosling-Goldsmith, 2018). Malengo haya 17 yanafungamana, yana uhusianifu na yanategemeana kiasi kwamba ufanisi wa moja utachangia mchakato wa kufikiwa kwa jingine (Barbier & Burgess, 2017). Makala haya yalichunguza malengo mbalimbali ya mpango wa MME yanayodhihirika katika tamthilia ya Shamba la Halaiki (2016).

**Kuhakikisha Afya Njema na Ustawi wa Watu wa Rika Zote**

Kwa kurejelea Shamba la Halaiki (Okello, 2016), wananchi wa jimbo la Matengo wanakabiliwa na magonjwa. Kulingana na Bi. Domo, watu wanaendesha na kuumwa na matumbo (uk.38). Kutokana na janga la mafuriko, Wanamatengo wanalazimika kuishi kambini. Wakiwa kambini, watoto wanakumbwa na maradhi kama vile kipindupindu na utapiamlo (uk.85). Badala ya Gavana Mbi kuwatafutia suluhu ya kudumu, anawapelekea fedha kidogo ili kuwafurahisha (uk.94, 85). Anafuja fedha zilizoidhinishwa kuwasaidia waathiriwa hawa.

Seneta Lila anawasaidia waathiriwa wa mafuriko kwa kuwapelekea dawa (uk.39). Hii ni njia mojawapo ya kuondoa magonjwa na kuhakikisha afya njema. Gavana mpya wa Matengo Bi. Cheupe anawapa wananchi msaada wa dawa na kuwahamisha kutoka maeneo ya chini hadi ya juu ili kuepuka gharika. Juhudi za viongozi hawa wawili: Seneta Lila na Gavana Cheupe zinaendeleza Lengo la 3 la mpango MME. Zinahakikisha kuwa raia wote wa jimbo la Matengo wanapata afya njema. Baada ya kuokolewa huku, wanaimba na kushangilia kupitia kwa ubeti wa pili wa shairi. Wanasema:

> *Kina mama wamefurahia, wanao wameponea,*
> *Watoto wanachekea, wazazi wao kubakia,*
> *Wagonjwa wameponea, wazee wametulia,*
> *Asante Seneta wetu, hakika umetusikia (uk.127).*

Mhimili wa pili wa nadharia ya Uhistoria Mpya unasisitiza umuhimu wa utunzi wa kazi. Shairi hili linabainisha furaha ya wakazi wa jimbo la Matengo wakiwemo watoto, wazazi na wazee baada ya viongozi Lila na Cheupe kusuluhisha tatizo la maradhi. Baada ya afueni hii, Wanamatengo wana ari kuwa hivi karibuni wakiongozwa na gavana mpya wataweza kutokomeza magonjwa kabisa (uk.127).

**Kuhakikisha Elimu Bora, na Yenye Usawa kwa Wote na Kutoa Fursa kwa Wote Kujiendeleza**

Katika *Shamba la Halaiki,* mafuriko yameathiri elimu ya watoto. Watoto wanajikuta kambini ambamo kuna njaa na magonjwa (uk.13). Mfumo wa kielimu wa jimbo la Matengo una tatizo, si elimu bora. Hii ndiyo maana watoto wa watu walio na uwezo wa kiuchumi hasa viongozi wanasomea katika nchi za ng'ambo. Watoto wa Fila na Gavana Mbi wanaishi na kusomea Marekani (uk.43). Vilevile, watoto wa Ndu'kuwili wanasomea ng'ambo (uk.76). Rajua, mwanawe Halaiki, alisomea Ufaransa. Kando na elimu katika jimbo hili kutokuwa bora, inaendeleza ubaguzi badala ya kuleta usawa. Watoto wa Wanamatengo wasio na uwezo wa kiuchumi wanakosa elimu kambini kwa sababu ya mafuriko (uk.13, 85).

Kiongozi wa jimbo anafaa kulipa suala la elimu kipaumbele. Gavana Mbi haweki mikakati yoyote kuimarisha elimu jimboni mwake. Badala yake anafisidi fedha za kuwasaidia waathiriwa wa mafuriko. Katika hali hii, mkewe Gavana Mbi anayeitwa Cheupe ndiye anatilia maanani suala la elimu. Anamwambia Gavana Mbi:

> *La, mume wangu! Hawa ni binadamu kama mimi na wewe…wanahitaji kuwasomesha wanao (uk.14).*

Kupitia muktadha huu, Cheupe anasisitiza kuwa watoto wote wa jimbo la Matengo wafaa kupewa elimu bora.

Kuhusu elimu, mwandishi anadhamiria kuonyesha dhima ya elimu. Elimu yafaa kuwapa wanafunzi macho ya kuona na akili ya kufikiri ili kutatua matatizo yanayokumba jamii. Licha ya Rajua kusomea uhandisi ng'ambo, macho na akili yake bado zimefumbwa. Hii ndiyo maana Halaiki ambaye ni babake anamwambia kuwa yeye ni kipofu na kuwa macho yake hayaoni rasilimali nyingi zilizo jimboni – kwamba jimbo la Matengo si maskini anavyofikiri; lina utajiri mwingi kama chemichemi za Mto Matengo, miti mirefu, mashamba yenye rutuba, migodi ya thamani na wanyama wa pori (uk.2–4).

**Kufikia Usawa wa Kijinsia na Kuwawezesha Wanawake na Wasichana Wote**

Katika *Shamba la Halaiki*, kuna wahusika wanawake. Hawa ni pamoja na: Cheupe, mkewe Gavana Mbi; Fila, mkewe Lila; Halima, mjakazi na msaidizi wa Gavana Mbi; Makini, dada wa Lila, Halaiki na Kizamani; Bi Domo, mwanamke anayeishi Bondeni na Bi Fedha, Waziri wa Fedha. Wanawake wanaonekana kukandamizwa na kubaguliwa. Cheupe ambaye ni mkewe Gavana Mbi anapopinga maovu ya mumewe, Gavana Mbi anamkaripia kwa hasira:

> *Toka uende nyumbani upike! Hata sijui kwa nini nilioa mtu asiyekuwa na kisomo kama wewe; zuzu wa mazuzu (uk.65).*

Kulingana na utamaduni wa Matengo, nafasi ya mwanamke ilikuwa jikoni. Jukumu lake kuu lilikuwa kupika na kumtunza mumewe. Kwa Mbi kumwamuru Cheupe aende nyumbani apike, anakumbuka mtazamo wa kitamaduni kuwa mwanamke hafai kushiriki katika masuala ya kisiasa. Daima anafaa kusalia nyumbani kutekeleza majukumu ya nyumbani yakiwemo kupika. Mbi anajuta kumwoa Cheupe eti hajasoma. Anamtusi. Hata hivyo, ukweli ni kuwa Mbi alimshawishi Cheupe asitishe masomo akiwa darasa la saba kinyume na maonyo ya wazazi wa Cheupe. Kutokana na hili, Mbi anamtusi mkewe kuwa ni zuzu wa mazuzu. Matusi dhidi ya mwanamke ni suala linalodididimiza hadhi yake. Isitoshe, Mbi anamnyoshea kidole Halima ambaye ni mjakazi na msaidizi wake na kumwambia Afisa: Niondolee hii takataka hapa (uk.47).

Ni kwa msingi wa utamaduni ambapo Kizamani anamnyooshea kidole Makini na kumkaripia: Nyamaza! Tangu lini mwanamke akaongea palipo na wanaume? (uk.67).

Inabainika kuwa utamaduni ulimfanya mwanamke akose sauti katika jamii; awepo tu kusikiliza bali asisikilizwe. Aidha, utamaduni unamdhalilisha mwanamke na kumfanya aonekane mtu duni asiye na uwezo. Fila anapomtazama Mbi kwa macho makali na kumnyoshea kidole, Mbi anamkumbusha kuwa kulingana na utamaduni mwanamke hawezi kumtisha mwanamume. Gavana Mbi anamwambia: Tangu lini mwanamke akanitisha mimi? (uk.49).

Aidha, utamaduni uliharamisha tendo la mwanamke kupewa urithi. Kizamani anapinga wazo la kumpa Rajua sehemu ya urithi wa babake. Anauliza swali la balagha: Tangu lini msichana akarithi mali ya babake? (uk.69).

Swali hili la balagha linaonyesha msimamo wa kitamaduni uliokuwa umekubalika katika jamii. Hii ndiyo maana Mzee Sikitu ambaye ni babake Lila, Kizamani na Halaiki anaunga mkono msimamo wa Kizamani ambao umesimikwa katika muktadha wa kitamaduni:

Japo ni mlevi, Kizamani amesema ukweli. Msichana hana haki ya kurithi mali katika utamaduni wetu (uk.69). Kando na kubaguliwa, mwanamke anadhulumiwa na kuteswa. Kwa amri ya Gavana Mbi, Afisa anamzaba kofi Halima ambaye ni mjakazi na msaidizi wa Gavana Mbi. Taswira inayochorwa kupitia kwa maelezo ya mwandishi inabainisha dhuluma dhidi ya Halima: Afisa anamzaba kofi zito linalomwangusha sakafuni. Anagaragara. Afisa anamvuta nje kwa mkono. Gavana Mbi anawatazama na kutabasamu (uk.47).

Mbi anataka kumpiga Fila baada ya tofauti baina yao kuzuka (uk.49). Cheupe anakiri kuwa amevumilia dhuluma kutoka kwa mumewe Mbi kwa miaka zaidi ya ishirini (uk.65). Fila anamtahadharisha Gavana Mbi:

Mimi si mkeo ambaye hunyamaza ukimfanyia kila madhila (uk.50).

Inabainika kuwa Cheupe amedhulumiwa kwa muda ila ananyamaza. Kizamani anaamka na kuelekea kwa Makini tayari kumzaba makofi (uk.67). Hapo ndipo Makini anamwambia Kizamani:

> *Unadhani mimi ni mkeo uliyemgeuza ngoma? Unadhani mimi ni mkeo ambaye huosha nguo hizo zako ulizokojolea? (uk.67).*

Kupitia maswali ya balagha na jazanda ya ngoma katika dondoo hili, Makini anatuchorea picha ya mkewe Kizamani. Hii ni dhuluma dhidi ya mwanamke katika asasi ya ndoa. Mapenzi linakuwa jukwaa la kumkandamiza mwanamke. Licha ya kuwa na mke, Gavana Mbi anashiriki mapenzi na Halima. Tokeo la mahusiano yao ya kimapenzi ni mtoto. Gavana Mbi anakosa kumtambua mtoto huyu na kumwonya Halima asimweleze mtu yeyote kuhusu uhusiano wao. Isitoshe, anamfuta kazi Halima wakati ambapo mumewe Halima amesombwa na mafuriko (uk.47). Baada ya kumfuta kazi Halima, Gavana Mbi anamwajiri Bi. Domo. Gavana Mbi anamweleza Afisa kuwa amempa Bi. Domo mwezi mmoja akubali kuhusiana naye kimapenzi, la sivyo amfute kazi (uk.81).

Inasemekana kuwa baba aliyemzaa Uma alimbaka bintiye Zuhura (uk.72). Hii inamfanya Zuhura kutaka kujiiua kwa kujitumbukiza majini (uk.73). Awali, mwanamke anaonekana mtu asiyeteta dhidi ya kudhulumiwa na kukandamizwa kwake. Cheupe anakiri

kuvumilia uasherati na dhuluma katika ndoa kati yake na Gavana Mbi kwa zaidi ya miaka ishirini. Miaka ishirini si muda mchache. Yamkini, Cheupe na Mbi wameishi katika ndoa kwa muda wa miaka ishirini na zaidi. Licha ya Cheupe kunyamaza na kuvumilia kwa muda huu, anazinduka na kuanza kutetea usawa na uhuru wake. Anasema:

> *Kweli, nimekuwa zuzu kubaki kimya… Lakini sasa macho yamefumbuka. Mjinga ameerevuka (uk.65).*

Cheupe tunayemwona katika muktadha huu ni jasiri kinyume na Cheupe mwanzoni mwa tamthilia ambaye ni mwoga. Halima anapompendekezea ajiunge na Lila ili kuwasaidia waathiriwa wa mafuriko, Cheupe anatingisha kichwa na kurusha mikono hewani akisema:

> *Hayo hayawezekani. Mume wangu atasema nini akisikia nimejiunga na wapinzani wake kuwasaidia watu? (uk.17).*

Cheupe tunayemwona mwishoni wa tamthilia sasa ni gavana mpya ambaye ni jasiri na tayari kutetea usawa wa kijinsia (uk.129).

Vilevile, Makini anapinga dhuluma kutoka kwa mwanamume Kizamani. Kizamani anapomzaba kofi, anamwambia kwa ukali:

> *Ungethubutu kunigusa, ningekuchafua sura. Unadhani mimi ni mkeo uliyemgeuza ngoma? Unadhani mimi ni mkeo ambaye huosha hizo nguo zako ulizokojolea? (uk.67).*

Isitoshe, anatetea usawa wa kijinsia anaposhikilia kuwa mwanamke ana haki ya kurithi mali ya wazazi katika jamii. Utamaduni wa Matengo haukumruhusu mwanamke kurithi mali. Mzee Sikitu ambaye ni babake Makini, Lila, Kizamani na Halaiki anasisitiza msimamo huu wa kitamaduni anaposema:

> *…msichana hana haki ya kurithi mali katika utamaduni wetu (uk.69).*

Makini anapinga maneno na msimamo huu wa babake kwa kusema:

> *Utamaduni unaomnyima msichana haki ya kurithi mali ya wazazi wake unarudisha maendeleo nyuma. Hata sisi (wanawake) tuna haki ya kunufaika na mali ya wazazi wetu na pia tunahitaji kupewa uwezo wa kujitegemea na kujenga jamii zetu (uk.69).*

Kupitia muktadha huu, Makini anajitokeza kama kiongozi anayetetea haki za wanawake. Anapinga mfumo wa kitamaduni ulioshusha hadhi ya mwanamke. Kulingana naye, kunyima wanawake haki kunadidimiza maendeleo. Hii ina maana kuwa maendeleo katika jamii yatapatikana wanawake wanapopewa nafasi sawa na wanaume. Babake anamweleza kuwa wanawake wataolewa na kusaidiwa na mabwana zao. Makini anaendelea kupinga msimamo huu. Anasema:

> *Enzi za wasichana kuolewa na kutegemea waume wao zimepitwa na wakati pia. Kwa sasa wanawake pia wanajitafutia riziki kama wanaume. Sisi tuna nafasi sawa katika jamii kama walivyo wavulana (uk.69).*

Inabainika kupitia Makini kuwa mwanamke amezinduka na kujitetea; kutetea nafasi yake katika jamii. Kando ya mwanamke kujitetea, anatetewa na wanaume. Hapa, Makini hatetei tu hali yake bali anatetea usawa wa kijinsia wa wanawake na uwezeshwaji wa wanawake.

Japo Mzee Sikitu anashikilia msimamo wa kitamaduni, anamshirikisha Makini katika kikao cha kufanya maamuzi muhimu ya kifamilia. Inabainika kupitia tendo hili kuwa mwanamke amejinasua kutoka kwa minyororo ya kitamaduni na kuanza kufanya maamuzi ya kuongoza familia na jamii. Uamuzi wa kumshirikisha Makini katika kikao hiki haukumfurahisha Kizamani ambaye anajaribu kumnyamazisha Makini.

> *Nyamaza! Tangu lini mwanamke akaongea palipo na wanaume? (uk.67).*

Bi. Kizee anamshauri Mzee Sikitu ayakubali mabadiliko katika jamii ambayo yanampa mwanamke haki ya kurithi mali (uk.71).

Halaiki, ambaye ni kiongozi wa familia, anamwezesha mwanamke kwa kumsaidia Zuhura ambaye ni mamake Uma. Baada ya kubakwa na babake mara kadhaa na

hatimaye kutiwa ujauzito, Zuhura alitaka kujitia kitanzi. Halaiki alimpata kando ya mto akiwa na lengo la kujitumbukiza majini akamwokoa na kumpa makao. Anamwoa Zuhura na kumkubali mtoto huyu kuwa wake. Zaidi ya haya, anaweka mambo haya kuwa siri. Jambo hili linadumisha heshima ya Zuhura na Uma jimboni (uk.73).

Lila ambaye ni Seneta wa jimbo la Matengo anatetea haki ya mwanamke kurithi mali. Anasema kuwa Rajua ana haki ya kurithi mali ya babake na afaa kupewa haki hiyo ili ajiamulie maisha yake (uk.69, 86, 87). Mwanamke anainuka kinyume na utamaduni uliomkandamiza na kuwa kiongozi. Bi. Cheupe anafanyika kuwa Gavana mpya baada ya Gavana Mbi kuondolewa mamlakani.

**Kuhakikisha Upatikanaji na Usimamizi Endelevu wa Maji na Usafi kwa wote**

Kwa kurejelea *Shamba la Halaiki*, jimbo la Matengo limeneemeshwa kuwa na Mto Matengo. Hata hivyo, usimamizi wa mto huu ni mbovu. Kulianzishiwa mradi wa kujenga bwawa katika mto huu ambao ungezuia mafuriko na kuzalisha nishati. Hata hivyo, mradi huu ulikwama miaka hamsini iliyopita. Mafuriko yanasababisha wananchi kuishi kambini. Kupitia maelezo ya Bi. Domo kwa Uma, uchafu umejaa kote. Uchafu huu umesababisha maradhi kama kuumwa na tumbo na kuendesha (uk.38). Aidha, hakuna maji safi (uk.38).

Seneta Lila anawaletea Wanamatengo walio kambini maji safi (uk.39). Kanisa kupitia kwa Ndu'kuwili vilevile linawapa waathiriwa wa mafuriko maji (uk.52). Mradi wa kuchimba mabwawa kumi ili kusambaza maji vijijini unakumbwa na ufisadi (uk.20).

**Nishati Mbadala kwa Gharama Nafuu**

Ingawa viongozi katika *Shamba la Halaiki* wana nguvu za umeme majumbani mwao, wananchi wengi wakiwemo akina Domo na Halima hawana (uk.5). Kinaya ni kuwa, japo kuna ukosefu wa nguvu za umeme, jimbo lina Mto Matengo ambao una mianguko ya maji inayoweza kutumiwa kuzalisha nishati mbadala. Rajua anasoma maandishi kwenye kibango:

> *Construction of Matengo dam to generate mega-hydroelectric power and control frequent flooding to be started in 196...potential hydroelectric power, constituting the world's asilimia 42 total…. (uk.4).*

Nishati asilimia arobaini na mbili ya nishati ya ulimwengu ingekuwa nishati kubwa mno. Bila shaka ingekuja kwa bei nafuu kwa Wanamatengo. Hata hivyo, mradi huu unakosa kuendelea kwa sababu ya uongozi mbaya. Viongozi wanafisidi fedha za kujenga mabwawa kumi. Mradi huu ungezalisha nishati mbadala ambayo ingekuwa ya bei nafuu (uk. 6–9).

Kwame Nkrumah ambaye alikuwa Rais wa kwanza wa Ghana kupitia hotuba yake alisisitiza kuwa bara la Afrika ni bara lenye rasilimali nyingi, nguvu kazi kubwa, na uwezo wa kipekee wa kuchangia maendeleo ya dunia. Kulingana naye, madini, mafuta, ardhi yenye rutuba, na nguvu kazi ya vijana ni vitu vilivyo na uwezo wa kufanya Afrika kuwa kitovu cha maendeleo ya dunia endapo vingetumika vizuri na ikiwa Afrika ingeungana na kushirikiana kwa pamoja (Nkrumah, 1963). Kwa kurejelea tamthilia ya *Shamba la Halaiki*, jimbo la Matengo sawa na bara la Afrika lina uwezo mkubwa wa kuzalisha nishati hivyo kuchangia maendeleo ya dunia. Tendo la Gavana Cheupe la kujenga mabwawa linadhihirisha jitihada za kuafikia L7 (uk.116).

**Kuweka Miji na Makazi ya Binadamu Kuwa Jumuishi, Salama, Imara na Endelevu**

Baadhi ya Wanamatengo katika tamthilia ya *Shamba la Halaiki* wameishi hemani kwa miaka zaidi ya hamsini kutokana na ukosefu wa makazi. Bikizee anakiri kuishi hemani tangu Matengo ijinyakulie uhuru (uk.9). Kuishi kwake hemani kwa miaka hamsini kunatokana na ukosefu wa makazi.

Makazi ya Wanamatengo yamesombwa kwa gharika. Hii inabainika kupitia ubeti wa kwanza wa shairi ambalo ni sauti ya wananchi wanaolia na kuomba msaada.

> *Kwa kite tunalia, gharika 'natumaliza,*
> *Watu wameangamia, mauti yatukereza,*
> *Mifugo na nyumba pia, maji*
> *'mekimbiza,*
> *Gavana wetu yu wapi? Msaada wako*
> *twahitaji (uk.13).*

Cheupe anapomweleza Gavana Mbi kuhusu matatizo ya waathiriwa wa mafuriko, Gavana Mbi anasema kuwa watapewa mahema. Mahema si makazi salama, imara wala endelevu. Ni makazi ya muda tu. Katika hali hii, Cheupe anajitokeza kushinikiza makazi salama, imara na

endelevu kwa wakazi wa Matengo. Anamwambia Gavana Mbi:

> *La, mume wangu! Hawa ni binadamu kama mimi na wewe. Wanastahili makao mapya ya kudumu (uk.14).*

Lila aliwasaidia Wanamatengo kwa kuwapelekea mahema (uk.39). Juhudi za kiongozi huyu zinaendeleza uafikiwaji wa L11.

**Kulinda Uhai Katika Ardhi**

Katika *Shamba la Halaiki*, jimbo la Matengo lina rasilimali nyingi. Utajiri wa jimbo hili unabainika kupitia mazungumzo kati ya Rajua na babake Halaiki. Rajua ana mtazamo kuwa hakuna kitu kizuri katika jimbo la Matengo. Halaiki anamzindua na kumwonyesha shamba lao ambalo lina rasilimali nyingi. Rajua anapoulizwa kilichomo shambani humo anasema:

> *Rotuba, miti mirefu, migodi ya thamani ya juu, wanyama wa pori, chemichemi ya Mto Matengo… (uk.2).*

Mbinu ya mdokezo iliyotumiwa hapa inaonyesha kuwa shamba hili lina rasilimali nyingi mno zisizoweza kuelezwa kikamilifu. Licha ya rasilimali hizi, uongozi mbaya wa Gavana Mbi unakosa kuwajibikia ulindaji wa uhai. Kwanza kabisa, uongozi huu unakosa kujenga mabwawa licha ya utabiri wa Bikizee. Mafuriko haya yanasababisha taswira mpya Matengo: harufu ya mizoga ya ndovu, mianguko ya miti mirefu kwenye chemichemi za Ziwa Matengo na maafa ya watu kumi (uk.24). Watu takribani elfu moja wanaangamizwa kwa mafuriko (uk.33).

Hata baada ya mafuriko kutokea, Gavana Mbi anakosa kuwashughulikia waathiriwa (uk.14). Anakosa kulinda uhai wa waathiriwa.

Kupitia swali la balagha, Bi. Domo anamuuliza Uma: Subira gani na watu wanakufa? (uk.38).

Sauti za watoto wa jimbo la Matengo zinasikika zikididimia:

> *Ng'eeeeeeee! Ng'eeeeee! Nataka mamiiiii,*
> *Ng'eeeeee! Ng'eeee! Nataka nyonyooo!*
> *Ng'eeee! Ng'eee! Nataka ujiii!*
> *Ng'ee! Ng'e! Nataka maji! (uk.53).*

Baada ya sauti za watoto kupotea, sauti za kina mama wa Matengo zinasikika zikididimia pia.

> *Uuuuwi! Usiniache mwanangu weeee!*
> *Uuuuwi! Fungua macho unitazameeee!*
> *Uuuuuwi! Ni wewe peke yakooo,*
> *Uuuuwi! Haki nakufuataaa (uk.54).*

Mbinu za takriri na nidaa zilizotumiwa katika sauti hizi za watoto na akina mama zinabainisha hali ya utamaushi kutokana na mafuriko.

Seneta Lila anachukua hatua kulinda uhai. Anawaletea waathiriwa chakula, dawa, mahema na maji safi (uk.39, 54). Aidha, Cheupe analinda uhai kwa kuandamana na Lila kuwapa msaada waathiriwa. Baada ya kuchaguliwa kama viongozi wapya wa Matengo, Cheupe na Uma wanachukua hatua ya kulinda uhai. Cheupe anawahamasisha na kuwahamisha Wanamatengo kutoka maeneo ya chini hadi ya juu. Tendo hili linawafanya waepuke kuathiriwa tena na mafuriko kwa kuwa mvua kubwa ilikuja kunyesha kulingana na utabiri wa Bikizee (uk.113). Isitoshe, kiongozi Cheupe anaanza mipango ya kujenga mabwawa ya kuzuia mafuriko siku za usoni (uk.116).

Kando na mauaji yanayotokana na janga la mafuriko, kuna mauaji yanayotokana na polisi. Watu zaidi ya kumi wanauawa na polisi katika maandamano (uk.29). Gavana Mbi na Fila wanapanga njama na kufaulu kumwua Halaiki ili Gavana Mbi apate Shamba la Halaiki (uk.42, 60). Walimtumia Kizamani ambaye ni kakake Halaiki kumwangamiza (uk.71). Bi. Fedha anatetea uhai baada ya kubadili mtazamo wake. Anamwambia Mbi:

> *Usimwage damu tena kakangu hasa ya watu waliokuauni kwa mvua na jua. Enough is Enough (uk.84).*

**Kuendeleza Jamii Jumuishi na Yenye Amani kwa Ajili ya Maendeleo Endelevu, Kutoa Haki kwa Wote na Kujenga Taasisi Imara zenye Kuwajibika katika Nyanja Zote**

Kwa kurejelea tamthilia ya *Shamba la Halaiki*, inadhihirika kuwa viongozi wa awali wa jimbo la Matengo waliweka mbinu kuhakikisha kuwa jamii ya Matengo ni jumuishi na yenye amani ili kuleta maendeleo. Mathalani, kuna sheria mbalimbali zilizowekwa ili kuhakikisha kuwa jamii hii ni jumuishi na yenye amani. Gavana Mbi anapomshauri Afisa kuwa angempiga mwanahabari aliyenasa picha ya ajuza ambaye alikuwa akipigwa na polisi, Afisa anamkumbusha kuwa mkono wa sheria ungempata. Hii ina maana kuwa kuna sheria inayothibiti uhuru wa wanahabari na vyombo vya habari (uk.30). Isitoshe, kuna katiba inayoongoza jimbo la Matengo (uk.31).

Hata hivyo, Gavana Mbi analenga kuondoa ujumuishi na amani katika jamii kwa kuziondoa baadhi ya sheria hizi. Anamwagiza Ndu'kuwili atayarishe mswada wa kudhibiti vyombo vya habari ili uende bungeni. Jambo linalobainika ni kuwa jimbo lilikuwa na katiba. Katiba ilitoa mwongozo kuwa ili patokee mabadiliko ya kisheria, sharti bunge liidhinishe kwa kuwa wabunge ni wawakilishi wa wananchi.

Sheria hii ililenga kuwa hakuna sheria ingepitishwa bila kujumuisha maoni ya wananchi ambao wanawakilishwa kupitia wabunge. Ndu'kuwili ambaye ni mshauri wa Gavana Mbi kuhusiana na masuala ya sheria anamshauri kuwa wabunge hawatakubali mswada huo kwa kuwa unakiuka katiba. Hata hivyo, Gavana Mbi yuko tayari kutumia ushawishi wake wa kisiasa kuondoa sheria inayohakikisha uhuru wa vyombo vya habari. Anamwambia Ndu'kuwili:

> *Zaidi ya nusu ya waheshimiwa hao ni wanachama wa chama changu tawala. Tayari waheshimiwa kutoka kabila letu wanaunga mkono mswada huo. Watawashawishi waheshimiwa kutoka kabila lile kuupitisha. Hakikisha kuwa hakuna chombo cha habari kitapeperusha habari bila idhini ya ofisi yako na kamishena. Tunaelewana? (uk.31).*

Uhuru wa vyombo vya habari unahakikisha kuwa kuna haki, amani na ujumuishi katika nchi. Kuondoa uhuru huu kungevuruga ujumuishi, haki na amani ya jimbo la Matengo. Kando na kuondoa baadhi ya sheria zinazoleta haki na ujumuishi katika jimbo, viongozi wakiongozwa na Gavana Mbi wanazikiuka baadhi ya sheria hizi (uk.43).

Inadhihirika vilevile kuwa kuna haki za kibinadamu. Gavana Mbi anashinikizwa kujiuzulu kwa kukiuka haki za binadamu (uk.28). Haki hizi zinalenga kudumisha amani ili jamii iwe jumuishi. Japo kuna haki hizi, Gavana Mbi anazikiuka hadharani. Anaruhusu polisi kutumia nguvu dhidi ya wananchi wanaoandamana kutetea haki zao bora tu wasiwe katika sare rasmi za polisi. Anamwambia Afisa:

> *Nimekuambia kila mara vijana hao wa Kabila Letu wasitumie nguvu wakiwa kwenye sare rasmi za polisi (uk.27). Nimekuambia kila mara unachohitaji kuwapa vijana hao ni mapanga na marungu. Sare za polisi na bunduki unawapa kwa amri ya rafiki yangu, Bwana kamishena (uk.27). Mngempiga mwanahabari huyo na kuharibu kamera yake jinsi mwenzako aliyetangulia alivyofanya mwaka jana (uk.27).*

Ili kuzuia kufukuliwa kwa dafina, Gavana Mbi anapanga njama na Fila za kuwalipa vijana ili wazue vurugu (uk.98–99). Kuna hali ya ubaguzi ambayo inazuia jimbo kuwa jumuishi. Ubaguzi huu ni wa kikabila. Bi. Fedha anamshauri Gavana Mbi wawape watu waliopoteza kadi za kupiga kura kadi hizo. Hata hivyo, Gavana Mbi na Bi. Fedha wanashikilia kuwa si wanajimbo wote wa Matengo watapewa. Kulingana nao, Wanamatengo wa kabila liitwalo Kabila Letu pekee ndio watakaopewa. Wale wa kabila liitwalo Kabila Lao hawatapewa. Huu ni ubaguzi. Kiongozi Fedha anasema: Kabila lile hatutawapa kadi za kupiga kura hata moja.

Ubaguzi huu unavuruga mshikamano wa jimbo hili. Inabainika kupitia Ndu'kuwili kuwa mwanamatengo aliyefuzu kuwa waziri wa fedha hakupewa kazi hiyo kwa kuwa hakuwa wa kabila lao au hakutoa hongo. Ndu'kuwili anamwambia Bi. Fedha:

> *Wewe mwanamke! Hustahili kuwa Waziri wa fedha hata! Aliyefuzu aliachwa eti kwa sababu hawezi kuzungumza kikwetu (uk.35).*

Japo kuna haki za kibinadamu katika jimbo la Matengo, haki hizi zinakiukwa. Lila anashikwa kwa tuhuma za kumwua Halaiki. Anatiwa gerezani bila hata kupewa nafasi ya kujitetea (uk.118–119). Inapogunduliwa kuwa hakuna ushahidi wa kutosha, anaachiliwa (uk.118). Gerezani, Lila anakosa huduma za kimsingi kama chakula, maji na choo. Isitoshe, chumba chenyewe ni kichafu na kina majambazi sugu na wauaji (uk.119). Hali hii ni kinyume na haki za wafungwa kwa mujibu wa Shirika la UM.

Kuna haki ya watoto kurithi mali ya wazazi wao. Kizamani anataka kurithi mali ya kakake Halaiki na anapinga Rajua na Uma ambao ni wanawe Halaiki kurithi mali ya baba yao. Fila mkewe Lila anamshinikiza Lila ambaye ni kakake Halaiki akubali kurithi mali ya Halaiki ili Uma na Rajua wasipate fursa ya kurithi.

Seneta Lila anajulikana kama mtetezi wa haki. Inapobainika kuwa Uma si mtoto wa Halaiki na kwamba utamaduni haumruhusu kurithi mali ya Halaiki, Lila anamtetea: Awe mwanaharamu au si mwanaharamu, yeye ni binadamu kama mimi na wewe. Anastahili kupata angalau sehemu ya mali ya Halaiki (uk.86). Inapobainika kuwa Rajua haruhusiwi na utamaduni kurithi mali ya babake kwa kuwa ni msichana (uk.69), Seneta Lila anamtetea: Rajua pia anastahili kuwa na mali yake binafsi ajiamulie maisha yake (uk.86).Kando na Lila, Makini ambaye ni dadake Lila, Halaiki na Kizamani anatetea haki ya Rajua kurithi mali ya babake (uk.68). Anapinga utamaduni unaomkandamiza mtoto msichana. Kulingana naye, utamaduni huu unarudisha nyuma maendeleo (uk.69). Bikizee vilevile anatetea haki za wasichana kama Rajua kurithi mali ya wazazi. Anasema:

> *Ili tujue kuwa mambo yamebadilika. Mtoto yeyote yule awe mwana aliyezaliwa nje ya ndoa au msichana ana haki ya kurithi mali. Ni vizuri twende na mabadiliko mazuri kama haya mwenzangu (uk.71).*
>
> *Haki na amani katika jimbo la Matengo inaafikiwa wakati sheria inaanza kuchukua mkondo wake (uk.109). Kuna mpango wa kumshtaki Gavana Mbi pamoja na maafisa wote wa serikali waliohusika katika ubadhirifu wa fedha za umma. Ndu'kuwili anawapa polisi ushahidi kutekeleza hili (uk.120).*

Katika hotuba yake, Cheupe anawauliza Wanamatengo:

> *Mko tayari kuhudhuria vikao vya mahakama, kesi za Mbi na Fila zitakapoanzishwa ikiwa watapatikana wakiwa hai? (uk.129).*

Cheupe anawahakikishia Wanamatengo kuwa kama Gavana mpya atahakikisha kuwa sheria imefuata mkondo wake na kwamba maovu ya viongozi wa awali kama Mbi yataanikwa (uk.129).

Halaiki anamwambia Rajua: Watazinduka, watatambua nguvu iliyopo katika umoja (uk.3).

Halaiki alikuwa na ndoto ya kuwepo jamii moja ya Matengo iliyo jumuishi na yenye mshikamano. Japo hali wakati wake ilionekana kuwa haiwezekani, baada ya kifo chake ndoto hii inatimia.

Baada ya Gavana na Seneta wapya kuchukua hatamu ya uongozi wa jimbo, umoja, mshikamano na ujumuishi unadhihirika (uk.130). Hotuba kati ya Seneta Uma na umati wa Wanamatengo inadhihirisha mshikamano wa jimbo ambalo awali lilikuwa limetengana kwa msingi wa ukabila:

> *Uma: Makabila mangapi yako hapa?Watu: Kabilamojaaa!Uma: Kabila gani hilo?*
> *Watu: Wanamatesngo walioungana. (uk.130).*

Tamthilia inapoanza tunaona jimbo lililo na makabila zaidi ya hamsini. Wakati wa uongozi wa Gavana Mbi, ukabila ulishamiri kote (uk.30). Wakati wa viongozi Cheupe na Uma, mshikamano unarejeshwa. Isitoshe, ghasia zinasitishwa; amani inashamiri (uk.130).

**Kuchukua Hatua Dhidi ya Mabadiliko ya Tabianchi**

Kwa mujibu wa TATAKI (2012), tabianchi ni hali ya hewa ya eneo fulani katika kipindi kirefu cha muda, inayojumuisha vipengele kama joto, unyevunyevu, upepo na mvua. Hivyo, mabadiliko ya tabianchi ni mabadiliko ya muda mrefu katika mifumo ya hali ya hewa ya eneo fulani, yanayoweza kujitokeza katika vipengele hivyo vya msingi vya tabianchi. Uendelevu wa kimazingira ni mhimili muhimu wa tatu wa Malengo ya Maendeleo Endelevu (MME), unaosisitizwa na wataalamu mbalimbali (Brodhag & Talière, 2006; Mensah, 2019).

Aidha, Kumar et al. (2014) wanabainisha kuwa mabadiliko ya tabianchi tayari yameanza kuathiri viumbe hai, ikiwemo kupungua kwa uzalishaji wa mazao na kubadilika kwa mifumo ya uhamaji wa wanyama.

Kwa kurejelea tamthilia ya *Shamba la Halaiki*, jimbo la Matengo limepitia mabadiliko ya tabianchi. Mafuriko yametokea (uk.13, 46); watu wameaga dunia kutokana na mafuriko haya (uk.13, 15, 24). Isitoshe, nyumba zimesombwa (uk.13). Inawalazimu Wanamatengo kuishi mahemani (uk.14, 39). Uongozi wa Gavana Mbi unakosa kuchukua hatua dhidi ya mabadiliko ya tabianchi. Japo ilipendekezwa kuwa mabwawa yajengwe kuzuia mafuriko (uk.20), Gavana Mbi na wandani wake wanatumia mradi huu kifisadi kujilimbikizia mali (uk.6–7). Mbi anafuja fedha za ujenzi wa mabwawa (uk.40).

Bikizee ambaye ni kiongozi wa Baraza la wazee anachukua hatua dhidi ya mabadiliko ya tabianchi kwa kutabiri kuwa kutakuwa na mvua kubwa ambayo itanyesha eneo la Matengo (uk.24). Bikizee ni kiwakilishi cha idara ya utabiri wa hewa ambayo hutabiri mabadiliko ya tabianchi. Anasema:

> *Kwa umbali naona mvua kubwa ikinyemelea. Mvua hiyo imeandamana na upepo mkali unaoweza kutingisha majabali. Italeta maafa mara kumi zaidi ya haya endapo hatua haitachukuliwa (uk.24).*

Kwa mujibu wa dondoo hili, tendo la kiongozi huyu wa kitamaduni kutoa utabiri huu ni juhudi mojawapo ya kuafikia L13. Cheupe ndiye Gavana mtarajiwa anayetarajiwa kuchukua nafasi ya Gavana Mbi. Uma ndiye Seneta mpya anayetarajiwa kuchukua nafasi ya Lila. Cheupe na Uma wanachukua hatua baada ya utabiri wa Bikizee. Wawili hao ni jazanda ya viongozi ambao huchukua hatua na kuweka mikakati ya kudhibiti mabadiliko ya tabianchi. Baada ya utabiri wa hali ya hewa kutolewa na idara husika, wanawahamisha watu kutoka mabondeni kuwapeleka katika nyanda za juu. Wanasema:

Uma:

> *Tunawaondoa watu kutoka hapa mabondeni na kuwapeleka katika nyanda za juu.*

Cheupe:

> *Mvua kubwa inatarajiwa wakati wowote kuanzia saa sita usiku. Imesalia nusu saa tu. Hatutaki mvua hiyo iwapate hapa msije mkasombwa tena (uk.113).*

Isitoshe, Cheupe ambaye ni Gavana mpya anaanza mipango ya kujenga mabwawa ili kuzuia mafuriko. Fila anamwashiria Gavana Mbi asome kibango. Maandishi ya kibango yanasema: Ujenzi wa mabwawa kando ya Mto Matengo ili kuzuia mafuriko na kuongeza nguvu za umeme utaanza keshokutwa punde tu dafina itakapofukuliwa chini ya Gavana mpya (uk.116). Matendo haya ya Cheupe na Uma ni mfano wa juhudi zinazotekelezwa na viongozi katika tamthilia ya *Shamba la Halaiki* ambazo zinalenga kuafikia L13.

## HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

**Hitimisho:** Kazi hii imewasilisha matokeo na mjadala kuhusu MME yanayobainika katika tamthilia ya *Shamba la Halaiki* (Okello, 2016). Kazi hii imebaini kuwa tamthilia ya *Shamba la Halaiki* ni jukwaa muhimu la kujadili maendeleo ya kijamii, kiuchumi na kimazingira. Hili limedhihirika kupitia vipengele vya kifasihi kama wahusika, mandhari na maudhui. Jumla ya Malengo 9 kati ya 17 yamebainishwa katika makala haya: L3, L4, L5, L6, L7, L11, L13, L15, L16. Matokeo haya yanaonyesha juhudi za jamii na viongozi katika kupambana na changamoto za kijamii, kiuchumi na kimazingira.

Hata hivyo, imegundulika kuwa malengo sita (L2, L8, L9, L10, L12 na L14) hayajapewa kipaumbele katika tamthilia hizi, jambo linaloashiria pengo katika uwasilishaji wa malengo haya sita: lishe bora, kazi zenye staha, viwanda, kupunguza utofauti, uzalishaji wenye uwajibikaji na kulinda uhai katika maji. Lengo la kumi na saba limejitokeza kama msingi wa utekelezaji wa malengo mengine kwa kuwa linahusu ushirikiano wa kimataifa katika kufanikisha MME.

**Mapendekezo:** Makala hii inapendekeza kuwa waandishi wa fasihi waendelee kuandika tamthilia zinazochunguza kwa kina masuala ya MME pamoja na uongozi bora. Jambo hili litasaidia jamii kutambua umuhimu wa maadili, usawa na uwajibikaji katika kuyafanikisha. Zaidi ya hayo, waandishi wanahimizwa kuibua na kuangazia kwa mapana masuala mahsusi kama lishe bora (L2), ajira zenye staha (L8), viwanda na ubunifu (L9), kupunguza pengo la kijamii na kiuchumi (L10), uzalishaji na matumizi yenye uwajibikaji (L12),

pamoja na uhifadhi wa uhai ndani ya maji (L14). Uandishi wa aina hii utachangia kwa kiasi kikubwa kuendeleza ajenda ya maendeleo endelevu katika jamii. Aidha, makala haya yanapendekeza kuwa watafiti wa baadaye waelekeze juhudi zao katika kuchunguza namna MME yanavyojitokeza na kufanikishwa katika tanzu mbalimbali za fasihi, si katika tamthilia pekee. Kwa mfano, tafiti zinaweza kupanuliwa ili kujumuisha riwaya, ushairi, hadithi fupi, pamoja na fasihi simulizi, ili kupata mtazamo mpana na wa kina zaidi kuhusu mchango wa fasihi katika kukuza na kueneza maendeleo endelevu.

**MAREJELEO**


Alcántara, S., Marín-Díaz, V., & Sola-Reche, J. M. (2020). Reading Harry Potter: A journey into students' understanding of sustainable development goals. *Sustainability, 12*(18), 7725. https://doi.org/10.3390/su12187725

Barbier, E. B., & Burgess, J. C. (2017). The sustainable development goals and the systems approach to sustainability economics. *Economics, 11*(1), 1–22. https://doi.org/10.5018/economics-ejournal.ja.2017-28

Brodhag, C., & Talière, S. (2006). Sustainable development strategies: The state of the art. *Sustainable Development*, *14*(2), 49–59. https://doi.org/10.1002/sd.281

Browne, E., & Millington, K. A. (2015). Social development and human development: Topic guide. GSDRC, University of Birmingham/HEART.

Brizee, A., & Tompkins, J. C. (2012). New historicism and cultural studies (1980s–present). Purdue University.

Creswell, J. W. (2003). *Research design: Qualitative, quantitative, and mixed methods approaches* (2nd ed.). Sage.

Edler, K. L., & Park, J. (2021). Culture and the sustainable development goals: An outlook of future opportunities (UNU Working Paper). United Nations University.

Gosling-Goldsmith, J. G. (2018). Sustainable development goals and uncertainty visualization (Unpublished master's thesis). University of Twente.

Greenblatt, S. (1980). *Renaissance self-fashioning: From More to Shakespeare*. University of Chicago Press.

Griggs, D., Stafford-Smith, O., Rockström, J., Öhman, M. C., Shyamsundar, P., Steffen, W., Glaser, G., Kanie, N., & Noble, I. (2013). Sustainable development goals for people and planet. *Nature, 495*(7441), 305–307. https://doi.org/10.1038/495305a

Havaldsen, G. (2020). Stories that change the way we see the world: Literature and the sustainable development goals. *Sustainability: Science, Practice and Policy, 16*(1), 1–12. https://doi.org/10.1080/15487733.2020.1765678

Kumar, S., et al. (2014). Impacts of climate change on biodiversity and ecosystems. *Journal of Environmental Studies, 12*(3), 115–128.

Magendane, K., & Kapazoglou, M. (2021). Approaches to study SDG interactions: Literature review of relevant frameworks. University of Amsterdam.

Mazrui, A. M., & Mazrui, A. A. (1995). *Swahili state and society: The political economy of an African language*. East African Educational Publishers.

Mazza, P. I. (2021). Concepts of sustainable development: A literature review and a systematic framework for connecting education with the sustainable development goals (SDGs). *International Journal of Humanities Social Sciences and Education, 8*(8), 106–112.

Mensah, J. (2019). Sustainable development: Meaning, history, principles, pillars, and implications for human action. *Cogent Social Sciences*, *5*(1), 1653531. https://doi.org/10.1080/23311886.2019.1653531

Mlama, P. M. (1991). *Culture and development: The popular theatre approach in Africa*. UNESCO.

Musindalo, M. A. (2020). Taswira ya haki za watoto katika riwaya teule za Kiswahili za milenia mpya (Unpublished master's thesis). Maseno University.

Mwanje, J. I. (2001). *Issues in social science research: Methodology series module 1*. OSSREA. https://www.ossrea.net/publications

Nkrumah, K. (1963, May 24). Speech at the founding of the Organization of African Unity (OAU), Addis Ababa, Ethiopia. https://www.au.int

Okello, D. (2016). *Shamba la halaiki*. Spotlight Publishers EA.

Taylor, P. (2016). The sustainable development goals and the millennium development goals: Bridging the gap. *Journal of Global Development Studies, 8*(2), 45–60.

TATAKI. (2012). *Kamusi ya Kiswahili sanifu*. Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Wamitila, K. W. (2006). *Yatima*. Vide-Muwa Publishers.